



## **Fahamu Haki Zako**

Mwongozo kwa Wazazi Wanaoishi na HIV

Machi 2017



Watu wote wana haki ya kufanya maamuzi yao wenyewe kuhusu uzazi, ikiwa ni pamoja na kuwa mjamzito na kuwa na watoto, haijalishi hali yao ya HIV. Nchini Canada, wanawake wanaoishi na HIV wanaendelea kuwa wajawazito na kupata watoto. Maendeleo katika matibabu ya HIV yamechangia katika kupunguza maambukizo ya HIV wakati wa ujauzito, wakati wa kujifungua na hata baada ya kujifungua.

Ujauzito na uzazi mara nyingi huandamana na hisia za furaha na matarajio na hata pia matukio ya dhiki na uoga wa kisichojulikana. Wazazi wanaoishi na HIV hukabiliwa na matatizo ya kipekee ambayo kwa kawaida huhusiana na maamuzi ambayo yanaweza kuwahatarisha maisha yao wenyewe na ya watoto wao. Baadhi ya wazazi wanaoishi na HIV huhukumiwa na kubaguliwa kutokana na maamuzi yao ya kuwa wajawazito na kupata watoto, inayosababisha ufikiaji wa misaada muhimu ya aina nyingi kuwa jambo muhimu. Hata hivyo, uwepo wa unyanyapaa unaohusiana na HIV, hutatiza uwezo wa ufikiaji na upataji usaidizi wa ujauzito na wa HIV kwa watu wenye HIV .

Kitabu hiki kiliandikwa kwa ajili ya wazazi au wazazi watarajiwa wanaoishi na HIV, ikiwa ni pamoja na wanawake, wanaume waliobadilisha jinsia na watu wasio na jinsia. Kinalenga kutoa maelezo halisi na kukuza ufahamu kuhusu baadhi ya maeneo muhimu ya wasiwasi ambazo wazazi wanaoishi au walioathiriwa na HIV wanazo.

Kitabu hiki kinatoa maelezo ya kisheria. Kumbuka kwamba watu na mashirika mengi tofauti yanaweza kukupa maelezo na usaidizi, lakini ni wakili *tu* anayeweza kukupa ushauri wa kisheria. Iwapo unahitaji ushauri wa kisheria kuhusu hali yako maalum, unapaswa kuwasiliana na wakili.

### **Je, kuna uwezekano upi wa kuambukiza HIV wakati wa ujauzito na kujifungua?**

Maambukizi ya moja kwa moja yamepunguzwa pakubwa nchini Canada kutokana na ufanisi wa matibabu ya kupunguza makali ya HIV. Kupata matibabu ya kupunguza makali ya HIV ukiwa mjamzito hupunguza uwezekano wa kumwambukiza kijusi au mtoto HIV hadi chini ya asilimia 2. Maambukizi yanaweza kupunguzwa zaidi hadi asilimia 0.4 wakati mzazi mwenye HIV ameanza matibabu ya kupunguza makali ya HIV zaidi ya wiki 4 kabla ya kujifungua.

### **Je, watu wanaoishi na HIV wanaweza kufunguliwa mashtaka kwa kukosa kuzuia maambukizi ya HIV kwa watoto wao wakati wa ujauzito?**

Hakujakuwa na kesi yoyote iliyoripotiwa nchini Canada ya mashtaka ya jinai dhidi ya mtu anayeishi na HIV kwa kutochukua hatua za kuzuia maambukizi ya HIV kwa watoto wao wakati wa ujauzito.

### **Je, mzazi anayeishi na HIV anapaswa kunyonyesha?**

Wazazi wanaoishi na HIV hukumbwa na changamoto tata kuhusu kuwalisha watoto wao. Kuna maelezo mengi yanayokinzana kuhusu kuwalisha watoto wachanga kwa wazazi wanaoishi na HIV na maelekezo yanayotofautiana duniani.

Heath Canada inahimiza kunyonyesha kama njia bora ya kuhakikisha kinga, ukuaji na maendeleo ya watoto wakubwa na wadogo. Ujumbe huu unakinzana na maelekezo ya kikliniki ya HIV na mapendekezo ya Canada kwa watu wanaoishi na HIV. Nchini Canada, inapendekezwa kwamba watu wanaoishi na HIV waepuke kunyonyesha na watumie fomula ili kuzuia maambukizi ya HIV, ambayo yanawezekana kupitia kunyonyesha.

Katika mwaka wa 2016, Shirika la Afya Duniani (WHO) lilikubali ushahidi unaoongezeka unaoonyesha kwamba kutumia dawa za kupunguza makali ya HIV kwa watu wanaoishi na HIV au watoto kunaweza kupunguza pakubwa hatari ya maambukizi kupitia kunyonyesha. Kwa mara ya kwanza, WHO ilipendekeza kwamba wazazi wenye HIV au watoto wao watumie dawa za kupunguza makali ya HIV katika kipindi chote cha kunyonyesha na hadi mtoto afike miezi 12. Hii ina maana kwamba mtoto anaweza kunufaika na kunyonya huku kukiwa na hatari ndogo ya kuambukizwa HIV.

WHO ilipendekeza kwamba mamlaka ya afya ya kitaifa kutoka kila nchi zirejeele ushahidi huu wakati wanabuni mikakati yao kuhusu kuwalisha watoto. Health Canada haikuwa imetoa maelekezo mapyayanayozingatia mapendekezo haya mapya ya WHO wakati kitabu hiki kilichapishwa.

### **Je, mtu anayeishi na HIV anaweza kufunguliwa mashtaka kwa kutochukua hatua za kuzuia maambukizi ya HIV kwa mtoto wake wakati wa kujifungua au kunyonyesha?**

Ni vigumu kuchukuliwa hatua za kisheria kutokana na unyonyeshaji, lakini inawezekana. Kuna mfano unaoonyesha kwamba mzazi anayeishi na HIV anayehatarisha kumwambukiza mtoto wake HIV wakati wa kujifungua na baada ya kujifungua (k.m., kwa kutowafahamisha wahudumu wa afya wanaomhudumia wakati wa kujifungua, kukataa dawa za kinga kwa mtoto mchanga, au kunyonyesha) anaweza kufunguliwa mashtaka ya jinai na hatua kuchukuliwa na mamlaka ya kuwalinda watoto.

Katika mwaka wa 2006, mwanamke kule Ontario alikiri kuwa na makosa ya *kukosa kupeana mahitaji ya maisha*. Wakati wa ujauzito, mwanamke huyu hakutumia dawa za kuzuia maambukizi ya HIV kwa mtoto wake. Hakuwafahamisha wahudumu wa matibabu kuhusu hali yake ya kuwa na HIV alipojifungua. Alimnyonyesha mtoto huyo, ambaye baadaye alipimwa na kupatikana kuwa na HIV.

Kwa kawaida, mashtaka ya kukosa kupeana mahitaji ya maisha huwa ya kesi za kuwatelekeza watoto. Katika kesi hii, kufungwa kwa mwanamke huyu hakukutokana na alichofanya au alichokosa kufanya wakati wa ujauzito wake, bali tabia yake baada ya mtoto kuzaliwa.

Ijapokuwa mashtaka ya jinai katika hali hizo huwa nadra na kwa kawaida huwa si kwa manufaa ya mtoto (uzingatiaji mkuu katika kesi za kuwalinda watoto), ni muhimu kujua kwamba hatua kama hizo za kisheria zinawezekana. Ni muhimu pia kufahamu kwamba,

hata wakati hakuna mashtaka ya jinai, mamlaka ya kuwalinda watoto yanaweza kuingilia kati katika hali ambayo wanaamini kwamba mtoto anahitaji ulinzi, inayomaanisha kwamba mtoto ameteseka au ako katika hatari ya madhara ya kimwili.

### **Je, ufichuzi ni nini?**

Ufichuzi, katika muktadha wa HIV, ni tendo rahisi la mtu kumwelezea mtu mwingine kuhusu hali yake ya HIV. Katika hali nyingi, watu wanaoishi na HIV hawana wajibu wa kisheria wa kufichua hali yao ya kuwa na HIV. Hata hivyo, sheria ya Canada inahitaji ufichuzi wa hali ya mtu ya kuwa na HIV kwa wapenzi wengine wa ngono, na katika hali nyingine finyu.

### **Je, wazazi wanahitajika kufichua hali yao ya kuwa na HIV au hali ya watoto wao ya kuwa na HIV kwa wahudumu wa jamii?**

Katika hali nyingi, wazazi hawahitajiki kufichua hali yao ya kuwa na HIV kwa wahudumu wa jamii, isipokuwa kama ufahamu wa hali ya HIV ya mzazi unahitajika ili kumlinda mtoto au mtu mwingine ambaye yuko katika hatari ya kuambukizwa.

Kuhusiana na wahudumu wa kuwalinda watoto, wahudumu hawa wamepewa mamlaka maalum na sheria za mkoa na za kitaifa ya kuwalinda watoto dhidi ya kutumiwa vibaya na utelekezaji. Katika hali nyingi, ufahamu wa hali ya HIV ya mzazi au mtoto si muhimu kwa wahudumu wa kuwalinda watoto kufanya kazi zao. Hata hivyo, masuala mengine yanayohusiana na HIV yanapaswa kuzingatiwa (k.m., kama mzazi au mtoto anatumia matibabu yanayopendekezwa na kupata huduma za usaidizi au kama hali mbaya ya kiafya au vipindi vya kutoweza vinaathiri uwezo wa mzazi wa kutimiza mahitaji ya mtoto wake). Ikiwa mtoto mwenye HIV anachukuliwa ili alindwe na shirika la kuwalinda watoto, taarifa ya kimatibabu ya mtoto huyo yanastahili kupeanwa kwa shirika hilo au mzazi mlezi ili kuhakikisha kwamba mtoto huyo anapokea matibabu na usaidizi bila matatizo.

Katika hali yoyote ambayo ufichuzi unahitajika kwa mhudumu wa jamii au mhudumu wa kuwalinda watoto, mzazi ana haki ya kuweka vikwazo na kufichua tu maelezo yanayofaa au kutoa kibali kwa wahudumu ili wafikie maelezo muhimu kutoka kwa mashirika mengine. Wazazi wanaweza kutafuta ushauri wa kisheria kabla ya kufichua hali yao kwa wahudumu wa jamii au wahudumu wa kuwalinda watoto na wanaweza kuomba kiasi fulani cha muda ili kufikiria kuhusu machaguo ambayo wanayo. Hata hivyo, maombi haya ya kueleweka hayawezi kutumiwa ili kuchelewesha mchakato na lazima yafuatiliwe kabisa.

### **Je, wazazi wanahitajika kufichua hali zao za kuwa na HIV kwa watoto wao?**

Wazazi hawahitajiki kufichua taarifa yao binafsi ya afya, pamoja na hali yao ya kuwa na HIV kwa watoto wao. Hii ni kwa sababu karibu mwingiliano wote wa nyumbani na majukumu ya wazazi hayana hatari yoyote halisi ya kuambukiza HIV. Iwapo mzazi atafichua hali yake, inapaswa kuwa ni uamuzi wake mwenyewe kufanya hivyo.

## **Je, watoto wanaweza kutenganishwa na wazazi wao kwa sababu ya mzazi kuwa na HIV?**

Hapana. Kuwa na HIV hakupaswi kutumiwa kama sababu ya msingi ya shirika la ustawi wa watoto kuhusika au mtoto kuchukuliwa.

## **Je, hali ya HIV huathiri mipango ya malezi au makazi?**

Haki na majukumu ya mzazi kwa mtoto wake hayabadiliki kwa sababu ya hali ya kuwa na HIV. Licha ya hayo, hali ya mzazi ya kuwa na HIV inaweza kuzingatiwa wakati wa kuamua makubaliano ya malezi, malipo ya kuwakimu watoto, au makazi msingi ya mtoto. Uzingatiaji mkuu katika kuamua mpango wa malezi au makazi kwa mtoto ni maslahi ya mtoto. Kwa hivyo, kwa mfano, ikiwa mzazi ana upungufu unaohusiana na HIV ambao unaathiri uwezo wake wa kumtunza mtoto wake, mapungufu haya na malezi mengine ya baadaye yanayohitajika ambayo lazima yapangwe ni masuala halali ya kuzingatiwa katika kuamua ni mipango gani ambayo inafaa maslahi ya mtoto.

Bado, hali ya HIV ya mzazi haipaswi kuwa kigezo bainishi cha kuamua mipango ya malezi au makazi. Hivyo basi, iwapo mzazi anahisi kwamba wapenzi wake wa zamani wanaweza kuwa wanatumia hali yake ya kuwa na HIV ili kumvunja moyo, kumuharibia jina, au kumnyanyapaa, basi mzazi aliyeathirika anapaswa kuzungumza na wakili au mhudumu wa usaidizi iwapo ukiukaji wa usiri unaweza kutokea. Ikiwa ukiukaji wowote wa usiri umetokea, katika hali hizi au vinginevyo, mzazi mwenye HIV aliyeathirika anapaswa kutafuta ushauri wa kisheria.

## **Je, ni lini wazazi wanapaswa kuwaeleza watoto wao kwamba watoto wana HIV na kuna hatari gani katika uwezo wa mzazi wa kufanya maamuzi kuhusiana na watoto wake?**

Hakuna umri wowote maalum ambao mzazi analazimika kisheria kumweleza mtoto kwamba anaishi na HIV lakini mtoto anapaswa kufahamishwa ifikapo wakati anaweza kufanya maamuzi yake mwenyewe ya matibabu. Hakuna umri uliowekwa ambapo mtoto anaweza kutoa kibali cha kupata huduma ya matibabu. Madaktari wanapaswa kutumia busara yao katika kila hali ili kuamua kama mtoto anaweza kutoa kibali. Mahakama yameamua kwamba watoto wa miaka tofauti wanaweza kutoa kibali. Kwa ujumla, watoto wanachukuliwa kisheria kuwa wanaweza kutoa kibali ikiwa wanaelewa hitaji la matibabu ya dawa, matibabu hayo yanahusu nini, na manufaa na hatari iwapo watapokea matibabu hayo.

Ikiwa mtoa huduma ya afya atafafanua mambo haya na aamue kuwa mtoto anayaelewa, na kwamba huduma ya afya ni bora kwa maslahi ya mtoto, mtoa huduma ya afya anaweza kumtibu mtoto bila kibali cha wazazi au walezi.

Kitu kingingine cha kuzingatia kuhusu wakati wa ufichuzi ni shughuli za kingono. Kwa kuwa HIV inaweza kuambukizwa kupitia ngono, vijana wanapaswa kufahamishwa

kuhusu hali yao ya kuwa na HIV kabla ya kuanza kujihusisha na ngono ili waweze kufanya maamuzi ya busara kuhusiana na shughuli zao za kingono na watimize majukumu yoyote yanayoibuka ya ufichuzi yaliyoainishwa na sheria ya jinai ya Canada.

### **Je, watoto wanapaswa kufichua hali yao kwa waalimu wao na/au wanafunzi wenza?**

Katika hali nyingi, hakuna jukumu la kisheria kwa watoto kueleza shule zao kwamba wana HIV na ni uamuzi wao kama watafichua maelezo haya au la. HIV haiambukizwi kupitia kugusana, kutapika, kutokwa na jasho, kinyesi, mkojo, machozi, au makamasi. Zaidi ya hayo, hakuna hatari ya kuambukizwa kutokana na kumkuna mtu mwingine au kupitia utemaji mate. Hata hivyo, ufichuzi unaweza kuwa wa maana, chini ya hali ambapo kufanya hivyo kunamwezesha kupata huduma na usaidizi wa HIV, au kumlinda mtoto huyo mwenye HIV.

### **Je, hali ya HIV ya mtoto itawekwa siri na shule yake?**

Katika tukio ambalo ufichuzi unahitajika, mamlaka ya shule inapaswa kuhakikisha kwamba idadi ndogo sana ya wafanyakazi wanaopaswa kujua ndio wanaofahamishwa kuhusu hali ya mwanafunzi. Ikiwa hali ya mwanafunzi imefichuliwa kwa mamlaka ya shule (k.m., mwalimu mkuu, mwalimu, mshauri, au wahudumu wa usimamizi), iwe kwa sababu mwanafunzi amefichua hali yake mwenyewe au kwa sababu mzazi au baadhi ya watu wengine wamefanya hivyo, mamlaka ya shule inapaswa kuweka maelezo hayo siri. Hali ya mtu huyo haipaswi kushirikiwa na wahudumu wengine wa shule. Ikiwa mwanafunzi ni mdogo, rekodi zake za matibabu haziwezi kufichuliwa na wahudumu wa shule bila kibali cha mzazi au mlezi wake.

Hata hivyo, jukumu hili la kisheria la usiri, halitumiki kwa wanafunzi wenza au mtu mwingine yeyote shuleni ambaye hana cheo chochote cha kirasmi. Sheria za usiri hazizuii sana mtiririko wa maelezo kati ya watu.

Katika baadhi ya mikoa (hasa, Alberta, Ontario, Newfoundland, Nova Scotia na Prince Edward Island), mamlaka ya shule yanawajibika kisheria kuripoti mwanafunzi shuleni ambaye ana au huenda ana HIV kwa Afisa wa Matibabu wa Mkoa wa Afya, ambaye ana jukumu la kuweka maelezo haya siri. Zaidi ya hayo, mamlaka ya shule yanaweza kurekodi hali ya HIV ya mwanafunzi katika rekodi zao, lakini maelezo haya yanapaswa kubakia tu na mhudumu anayefaa katika mfumo salama wa kuweka faili ili kulinda faragha ya mwanafunzi.

### **Je, shughuli za mwanafunzi zitawekwa vikwazo kwa sababu amefichua hali yake ya HIV?**

Kutokana na hatari finyu ya kuambukiza HIV kupitia kugusana, mwanafunzi anapaswa kushiriki katika shughuli bila vikwazo vyovyote. Bado shule itahitajika kuchukua tahadhari za kawaida katika shughuli zote ambazo zinahusisha kugusa damu au ugiligili

wa mwili. Hata hivyo, Afisa wa Matibabu wa Afya katika mkoa au himaya husika huenda akapata kwamba kuna hali maalum ambazo zinaweza kusababisha vikwazo fulani.

Ikiwa mwanafunzi anahitaji malazi maalum, shule ina jukumu la kutimiza hitaji hili hadi katika kiwango cha “ugumu usiostahili.” Kiwango cha ugumu usiostahili kiko juu, na shule inayodai ugumu usiostahili ina jukumu la kuthibitisha; hiyo ni, lazima shule itoe ushahidi wa kutosha wa kuunga mkono madai yake kwamba hitaji la mtoto wako la malazi linasababisha ugumu usiostahili. Ijapokuwa, kuongea kwa ujumla, ili kusaidia shule kutimiza mahitaji ya mtoto, mwanafunzi anapaswa kutoa maelezo kuhusu mahitaji yake yanayohusiana na HIV. Hata hivyo, ufichuzi au utambuzi wa hali halisi ya mwanafunzi ya HIV hauhitajiki wala sio muhimu.

## **NYENZO ZA ZIADA**

Bitnun et al., “Prevention of vertical HIV transmission and management of the HIV-exposed infant in Canada in 2014,” *Canadian Journal of Infectious Diseases and Medical Microbiology* 25, 2 (March/April 2014): 75–77.

Canadian HIV/AIDS Legal Network, *Disclosure in School and Daycare*, 2014.

Canadian HIV/AIDS Legal Network, *Disclosure, Privacy and Parenting*, 2014.

P. Khosla, A. Ion and S. Greene, *Supporting Mothers in Ways that Work: A Resource Toolkit for Service Providers Working with Mothers Living with HIV*, The HIV Mothering Study Team & The Ontario Women’s HIV/AIDS Initiative, January 2016.

Society of Obstetrics and Gynaecology of Canada Clinical Practice Guideline, *Canadian HIV Pregnancy Planning Guidelines*, No. 278, June 2012.

Society of Obstetrics and Gynaecology of Canada Clinical Practice Guideline, *Guidelines for the Care of Pregnant Women Living With HIV and Interventions to Reduce Perinatal Transmission*, No. 310, August 2014.

## **SHUKRANI**

Mwongozo huu umetengenezwa na Canadian HIV/AIDS Legal Network. Ufadhili umetolewa na Public Health Agency of Canada.

Mtandao wa Kisheria unamshukuru sana Saara Greene na Jessica Whitbread kwa mchango wao wa thamani katika kitabu hiki.